

**HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA,  
UTAMADUNI NA MICHEZO, MHE. DKT. FENELLA E.  
MUKANGARA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA  
KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**



## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Asasi zake katika mwaka wa fedha wa 2015/2016.
2. **Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa unaoniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu niliyokabidhiwa na Mhe. Rais mwaka 2012 ya kulitumikia Taifa letu.
3. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutuongoza vyema katika Awamu ya Nne ya Serikali tangu mwaka 2005 hadi mwaka huu wa 2015. Ni matumaini yetu kuwa tutapata tena Rais mwingine msikivu na mchapakazi atakayetuongoza vyema katika Awamu ya Tano.

4. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake shupavu na makini. Ni matumaini yetu kuwa busara na uchapakazi wake bado unahitajika katika kuendelea kuiongoza Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar.
5. **Mheshimiwa Spika**, nitumie nafasi hii kuwapongeza viongozi wengine wa Kitaifa ambao wameiwezesha Awamu ya Nne kwa upande wa Bara na Awamu ya Saba kwa upande wa Zanzibar kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Viongozi hao ni pamoja na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.
6. **Mheshimiwa Spika**, vilevile nawapongeza Mawaziri wote wanaoendelea kuiwezesha Serikali ya Awamu ya Nne kutekeleza majukumu yake na hasa hoja zao walizowasilisha hapa Bungeni. Pongezi hizi zinaanza kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kwa hotuba yake fasaha yenye maelezo ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

7. **Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kuwapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri wanayoifanya kuishauri Wizara katika maeneo mbalimbali. Wizara itaendelea kutekeleza ushauri unaotolewa. Shukrani na pongezi zangu za dhati ziende kwa Mwenyekiti, Mhe. Said Mtanda (Mb) na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Albert Obama (Mb). Kwa ushauri wao ambao umefanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara.
8. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wapya walioteuliwa na Rais kuongoza Wizara mbalimbali hivi karibuni.
9. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi kwa Wabunge wapya walioteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambao ni Mhe.  
Dkt. Grace Puja na Mhe. Innocent Sebba.

- 10. *Mheshimiwa Spika*,** nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza wabunge wenzangu kwa jinsi mnavyojitoa katika kudhamini matamasha, mabonanza na mashindano ya michezo kwa vijana mbalimbali katika majimbo au maeneo yenu ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vyia michezo kwa timu mbalimbali.
- 11. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, hususan wananchi wa Jimbo la Mbanga Magharibi kwa kuondokewa na Mbunge wao Mhe. John Komba ambaye pia alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii aliyefariki tarehe 28 Februari 2015. Aidha, napenda kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, hususan wananchi wa Jimbo la Magomeni, Zanzibar kwa kuondokewa na Mwakilishi wao Mhe. Salmin Awadh tarehe 19 Februari 2015.
- 12. *Mheshimiwa Spika*,** Pia ninatoa pole kwa wananchi wote waliopoteza ndugu zao

kutokana na majanga na maradhi mbalimbali yaliyotokana na ajali za barabarani maeneo mbalimbali nchini, mafuriko, majanga ya moto hususan Vijana wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hosteli za Mabibo bila kuwasahau wanamichezo, wasanii na wanahabari wote waliopoteza maisha yao katika siku za hivi karibuni. Ni matumaini yangu kuwa tatizo kubwa la ajali za barabarani litapatiwa ufumbuzi na mamlaka zinazohusika, ili kuokoa maisha ya watanzania wengi yanayopotea. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

## B. MAJUKUMU YA WIZARA

**13. *Mheshimiwa Spika***, Wizara inatekeleza majukumu ya msingi ambayo yanajumuisha:-

- i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo;
- ii. Kuratibu na kusimamia masuala ya maendeleo ya vijana;
- iii. Kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali na kusimamia Vyombo vya Habari nchini;
- iv. Kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni nchini;

- v. Kuratibu na kusimamia maendeleo ya michezo nchini;
- vi. Kusimamia utendaji kazi wa Asasi, miradi na programu zilizo chini ya Wizara; na
- vii. Kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara.

### C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2014/2015

#### Mapato na Matumizi

- 14. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi **1,149,008,000** kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya shilingi **811,616,116** zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia **71** ya lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Mchanganuo wa makusanyo upo kwenye **Kiambatisho Na. I.**
- 15. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilitengewa shilingi **19,806,611,000** ikiwa ni Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara). Fedha hizo zinajumuisha

- (i) Mishahara ya Wizara (PE)  
Shilingi **3,151,654,000**
- (ii) Mishahara ya Asasi (PE)  
Shilingi **7,849,270,000**
- (iii) Matumizi Mengineyo ya Wizara (OC)  
Shilingi **5,265,687,000**
- (iv) Matumizi Mengineyo ya Asasi (OC)  
Shilingi **3,540,000,000**

Hadi mwezi Aprili, 2015 shilingi **14,446,963,490** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia **73** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo ni shilingi **4,864,434,620** na shilingi **9,582,528,870** ni Mishahara.

### **Miradi ya Maendeleo**

**16. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilitengewa shilingi **16,850,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 shilingi **7,000,000,000** zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia **42**. Kati ya fedha zilizopokelewa, zilizotumika ni shilingi **6,637,953,520**. Miradi iliyotekelizwa ni pamoja na Upanuzi

wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo (Uboreshaji wa Uwanja wa Uhuru) na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

## **SEKTA YA HABARI**

- 17. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa Fedha 2014/2015 Wizara imeendelea kusimamia Sekta ya Habari na Utangazaji kikamilifu licha ya changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika sekta hii. Mionganoni mwa changamoto hizo ni kuongezeka kwa mifumo na njia za mawasiliano kwa umma kama mitandao ya kijamii kwenye Intaneti kunakoathiri maudhui ya taarifa zinazotolewa.
- 18. *Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto hizi Wizara kwa kushirikiana na Kamati ya Maudhui (TCRA) imevitembelea vituo mbalimbali vyataga utangazaji kwa madhumuni ya kutoa elimu kwa wamiliki na watumishi wa vyombo hivyo. Aidha, Kamati ya Maudhui imeendesha warsha za kuwakutanisha wadau wa maudhui wa kujitegemea, wamiliki wa vituo vyataga utangazaji na wamiliki wa miundombinu ya dijiti ili kuwapa fursa ya kutoa mchango wao katika kuboresha vipindi mbalimbali vinavyorushwa kupitia mfumo wa utangazaji wa digiti.

- 19. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kuisemea Serikali katika kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu utendaji wa Serikali kwa wananchi. Vilevile Wizara imeendelea kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza katika Vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii.
- 20. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeratibu programu ya kuvijengea uwezo Vitengo vya Mawasiliano Serikalini katika Wizara, Serikali za Mitaa, Wakala za Serikali na Taasisi za Umma kwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara ili Maafisa Mawasiliano hao waweze kuzisemea na kutoa ufanuzi kwa umahiri mkubwa masuala yanayohusu taasisi zao. Kwa minajili hiyo, Wizara iliratibu kikao kazi kilichofanyika Mkoani Mtwara na kuhudhuriwa na Maafisa Mawasiliano 270. Kikao hicho kililenga kuwaelimisha Maafisa hao mbinu za ufuatiliaji wa maudhui katika mitandao ya kijamii, mawasiliano ya kimkakati, namna bora ya kuandika hotuba na masuala ya kiitifaki.
- 21. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendeleza uhuru wa Vyombo vya Habari kipindi cha Januari hadi Aprili, 2015 Wizara imeendelea kusajili magazeti na majarida 21 na kufanya jumla ya magazeti na majarida yaliyosajiliwa

nchini kufikia 849. Katika kuendeleza uhuru huo wa habari, Wizara imeratibu ushiriki wa vyombo vyahabari katika matukio mbalimbali ya Kiserikali, yakiwemo ya Vikao vyahabari, Sherehe za Kitaifa za Uhuru na Muungano na ziara za Viongozi Wakuu wa Nchi za nje.

**22. *Mheshimiwa Spika*,** kama nilivyoahidi mbele ya Bunge lako tukufu la Bajeti la mwaka 2014/2015 kwamba, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara itawasilisha Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari, nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa muswada wa Sheria hiyo umesomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa 19 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muswada huo ukipitishwa kuwa sheria utaweka misingi imara katika kufanya taaluma ya Uandishi wa Habari na Utangazaji kutambulika na kuboresha mazingira ya utendaji kazi ya watumishi katika Vyombo vyahabari.

**23. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) lina wajibu wa kutoa huduma za habari kwa wote, hivyo katika kipindi cha 2014/2015 Shirika limeweza kurusha matangazo ya moja kwa moja ya Bunge la kawaida la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge Maalum la Katiba kupitia chaneli zake za Radio na Televisheni. Aidha,

TBC imeendelea kuandaa na kurusha vipindi maalum kwa ajili ya kuelimisha umma; vipindi hivyo ni kama vile vinavyoitangaza Katiba Inayopendekezwa kifungu baada ya kifungu wakati wa taarifa za habari.

- 24. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imeendelea na mchakato wa kukamilisha mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji na sasa ipo katika hatua za mwisho za kupata mkopo wa kugharamia mradi huu toka benki ya Rasilimali Tanzania (TIB).
- 25. *Mheshimiwa Spika*,** baada ya TSN na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuingia mkataba wa ubia wa kuendeleza kiwanja kilichopo Kitalu Namba 27, Central Business Park Dodoma, kwa ajili ya kujenga jengo la kupangisha, ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba tayari Mshauri Mwelekezi amepatikana kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.
- 26. *Mheshimiwa Spika*,** naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Nchi yetu Tanzania ni moja kati ya nchi zilizofanikiwa kuhamia katika mfumo wa utangazaji wa dijiti kabla ya tarehe 30 Juni, 2015, muda wa mwisho uliowekwa na Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU). Mamlaka ya Mawasiliano

(TCRA) imesimamia vizuri zoezi hili na mji wa Lindi ulikuwa wa mwisho kuzima mitambo ya analoji hapo tarehe 30 Aprili, 2015.

## **SEKTA YA MAENDELEO YA VIJANA**

**27. *Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Maendeleo ya Vijana ni muhimu katika kujenga na kuboresha mazingira kwa ajili ya ustawi wa vijana. Katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya vijana, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo baadhi ya Halmashauri kutoanzisha SACCOS na kutotenga asilimia tano (5%) ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha vijana.

Changamoto nyingine ni mitizamo hasi ya vijana kutaka kuajiriwa badala ya kujiajiri wenyewe, vijana kutohamasika na kutumia fursa zilizopo ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kuendeleza miradi yao kwa kupata mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Aidha, changamoto nyingine ni pamoja na kukosa maarifa ya kubuni mawazo bora ya biashara yanayowawezesha kukopesheka.

**28. Mheshimiwa Spika,** katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizi, Wizara imeendelea kuwajengea vijana uwezo kwa kuwapa mafunzo na ujuzi katika maeneo mbalimbali. Maeneo hayo ni pamoja na uongozi, uandaaji wa maandiko bora ya miradi, stadi za maisha, utunzaji wa vitabu vya mahesabu na kumbukumbu za biashara pamoja na kujenga tabia ya kuweka na kukopa kupitia SACCOS za vijana zilizoanzishwa katika Halmashauri husika.

Aidha, jumla ya vijana 1550 kutoka katika Mikoa ya Mara (205), Arusha (88), Mbeya (403), Dodoma (198), Kilimanjaro (73), Kigoma (161), Ruvuma (284) na Singida (188) wamepatiwa mafunzo hayo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015.

**29. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu Mfuko wa Maendelo ya Vijana ili kuhakikisha kuwa vijana wengi wanapata mitaji ya kuanzisha au kuendeleza biashara zao kwa kuwapatia mikopo yenyenye masharti nafuu.

Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 jumla ya Shilingi 6,000,000,000 zilitengwa kwa

ajili ya Mfuko huo. Hadi Aprili, 2015, Wizara ilipokea kiasi cha Shilingi 2,000,000,000. Fedha zilizokopeshwa kwa vikundi vya vijana kwa ajili ya kuendeleza biashara zao ni shilingi 1,637,953,520. Hata hivyo, Wizara inaendelea kupokea na kuchambua maombi ya mikopo kutoka Mikoani ili kukamilisha kiasi kilichobaki cha fedha.

- 30. *Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha mikopo kwa ajili ya vijana inatolewa kwa wakati kwa wale walioomba, Wizara inaendelea kuhamasisha vijana nchini waweze kutumia fursa hii kwa kuomba mikopo, kutoa mafunzo kwa vijana, kuharakisha uchambuzi wa maandiko ya miradi yanayowasilishwa kwa ajili ya mikopo pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Mfuko. Lengo ni kuharakisha shughuli za utoaji mikopo pamoja na kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inarejeshwa kwa wakati.
- 31. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwezi wa Desemba, 2014 hadi Aprili, 2015 Wizara ilifanya tathmini ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Tabora, Tanga, Morogoro na Mtwara. Matokeo ya tathmini hii yalionesha kwamba vijana wengi walionufaika na mikopo

kupitia mfuko huu wanafanya vizuri katika kuendesha Miradi yao ambayo imewapatia ajira na kuwaongezea pato lao kiuchumi. Waheshimiwa wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii nao wametembelea na kukagua miradi ya vijana katika baadhi ya Halmashauri na kutoa ushauri wa kuboresha matumizi ya Mfuko huo.

- 32. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhamasisha maendeleo ya wananchi, kudumisha umaja, amani, upendo na mshikamano wa kitaifa kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru. Kwa mwaka 2014, Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizinduliwa tarehe 2 Mei Mkoani Kagera. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo alikuwa Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho ya kilele cha mbio hizo yalifanyika mkoani Tabora tarehe 14 Oktoba, 2014 na Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia mbio hizo, jumla ya miradi ya maendeleo 1,451 yenye thamani ya shilingi 361,384,288,194 ilikaguliwa, kuzinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi.

- 33. *Mheshimiwa Spika***, maadhimisho ya kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2014 yalifanyika sambamba na maadhimisho ya Wiki ya Vijana kitaifa. Maadhimisho haya yalianza rasmi tarehe 8 Oktoba na kuhitimishwa tarehe 14 Oktoba, 2014 mkoani Tabora. Lengo la maadhimisho hayo ni kuwakutanisha vijana kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini na kuwapa fursa za kujifunza, kubadilishana uzoefu, ujuzi, kuonyesha vipaji na ubunifu wa kazi zao, pamoja na kujenga mtandao na wadau mbalimbali wa maendeleo ya vijana.
- 34. *Mheshimiwa Spika***, maonesho katika Wiki ya Vijana yalishirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Asasi za kiserikali na zisizo za kiserikali, Vikundi vya Vijana Wajasiriamali, Asasi za Kibenki na Asasi za Kimataifa ambazo ni ILO, UNFPA, AMREF na BALTON Tanzania. Aidha, Vijana 250 walishiriki katika midahalo ya kuwajengeta uelewa wa masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya vijana. Masuala yaliyojadiliwa ni nafasi ya kijana katika kujenga umoja wa kitaifa, dhana ya kujitolea na kujitegemea, utunzaji wa mazingira fursa za ajira na afya ya uzazi kwa vijana.

## SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

- 35. *Mheshimiwa Spika*,** Utamaduni umekuwa chombo cha kuhimiza jamii, kuthamini na kutumia ujuzi, taaluma na teknolojia ya kisasa na ya jadi katika kuimarisha afya, matumizi bora ya mazingira, rasilimali na kuendeleza jamii. Hata hivyo, kumejitokeza changamoto ya dhana potofu ya kutumia viungo vya binadamu wenzetu kama kwamba ndio tiba na dawa ya kujiongezea utajiri. Hii ni dhana potofu inayovunja misingi ya utamaduni ikiwamo haki za binadamu na utu. Dhana hii inatakiwa kupingwa na kila mwana jamii nchini kwa kutambua kuwa binadamu wote ni sawa. Changamoto nyingine zilihusu kasi ndogo ya ukamilishaji wa kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na uwezeshaji finyu wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.
- 36. *Mheshimiwa Spika*,** licha ya changamoto zinazoikabili Sekta ya Utamaduni, Wizara, pamoja na mambo mengine, imefanikiwa kufanya utafiti wa msamiati wa lugha za jamii, utafiti wa majina fiche 1800 ya lugha za asili katika Mikoa sita ya Tanzania Bara ambayo ni Morogoro, Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara

na Dar es Salaam. Wizara pia imeratibu na kusimamia mchakato wa uanzishwaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo Makao yake Makuu yatakuwa katika jengo la iliyokuwa “Eastern African Centre for Research on Oral Traditions and African National Languages (EACROTANAL)”, Zanzibar.

**37. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara, kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliandaa na kurusha hewani vipindi 40 vya Lugha ya Taifa kupitia redio ya TBC<sub>Taifa</sub>, vipindi 40 vya “Kumepambazuka” kupitia Radio One na vipindi 40 vya Ulimwengu wa Kiswahili kupitia televisheni ya TBC<sub>1</sub>. Vipindi hivi hulenga, kuelimisha Umma wa Watanzania juu ya makuzi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili, vikiwemo msamiati, sarufi na fasihi yake. Vile vile Baraza lilisoma miswada 20 ya vitabu vya taaluma na kuvipatia Ithibati ya Lugha.

**38. *Mheshimiwa Spika*,** Baraza la Kiswahili la Taifa limefuatilia matumizi ya Kiswahili na kubaini makosa mbalimbali yaliyofanywa na Vyombo vya Habari na watumiaji wengine wa Kiswahili na kuyasahihisha kwa kutoa

ushauri wa matumizi stahiki. Baraza katika kujiimarisha, limeongeza wigo wa kiutendaji kwa kuandaa Kamusi Kuu na kufanya warsha nne za uandishi wa fafanuzi za maneno (utomeshaji). Aidha, kitabu cha *Furahia Kiswahili kwa Wageni* kimeandaliwa na tayari nakala 5000 zimechapishwa.

- 39. *Mheshimiwa Spika*,** Baraza pia limeratibu na kutoa huduma za tafsiri kwa asasi za serikali, mashirika ya umma, pamoja na watu binafsi. Aidha, Baraza limetoa huduma ya ukalimani kwenye mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika huko Malabo-Equatorial Guinea, mwezi Julai 2014, pamoja na mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika huko Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Januari 2015. Vilevile, Baraza lilihimiza upanuzi wa matumizi ya Kiswahili ndani na nje ya nchi, jambo lililowezesha kuanzisha mafunzo ya lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu kadhaa vya Afrika na hivyo kutoa pia fursa za ajira kwa watalaan wa Kiswahili wa Tanzania.
- 40. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliendelea kukusanya taarifa mbalimbali za Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kwa kufanya mahojiano na wazee

walioshiriki katika harakati za Ukombozi na kupata ushuhuda wao. Hadi Aprili, 2015 Wazee 20 wamesha hojiwa na baadhi ya maeneo yenye historia ya harakati za ukombozi yamepigwa picha. Taarifa hizi zitatumika kuandaa vipindi vyta televisheni na redio kwa lengo la kuelimisha wananchi kuhusu historia ya ukombozi wa nchi yetu na Bara zima la Afrika.

- 41. *Mheshimiwa Spika*,** utafiti wa mila na desturi za jamii tano umefanyika. Jamii hizo ni:- Wazigua, Wasukuma, Wameru, Wakwere na Wabarbeig na matokeo yake yamehifadhiwa kwa njia ya TEHAMA na kuwekwa kwenye tovuti kuu ya Serikali ili kuyasambaza kwa jamii pana ya Watanzania. Utafiti huu ni endelevu na unalenga kuzifikia jamii nyinginezo nchini.
- 42. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara pia iliratibu ushiriki wa vikundi vyta ngoma za asili na fani nyingine katika Maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa, hususanimiaka 53 ya Uhuru na miaka 51 ya Muungano, ambapo wasanii wapatao 276 kutoka mikoa ya Kigoma, Mara, Mbeya, Mwanza, Mtwara na Zanzibar walishiriki. Wasanii hawa waliweza kutoa ujumbe wa kauli mbiu za maadhimisho kwa wepesi na ufanisi kupitia ngoma za asili na nyimbo za

kwaya. Kauli mbiu hizo zilihusu kuhamasisha Watanzania wajitokeze kuipigia kura Katiba Inayopendekezwa na kushiriki kwenye Uchaguzi Mkuu. Aidha, Wizara ilisimamia uendeshaji wa Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania lilofanyika Bagamoyo na kuhudhuriwa na vikundi 34 vya kitaifa na vikundi vitatu vya kimataifa.

- 43. *Mheshimiwa Spika***, zaidi ya hayo, Wizara imeratibu mkutano wa Sekta ya Utamaduni uliofanyika mwezi Machi, 2015. Mkutano huo ulilenga kuwahimiza wadau wa utamaduni kutumia fani za sanaa kuwaelimisha Watanzania maudhui ya Katiba Inayopendekezwa.
- 44. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) liliendesha mafunzo ya utambaji hadithi, ngoma za asili na uchoraji, kwa watoto 100 wa shule za Msingi na watoto 100 kutoka mazingira magumu kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji vyao katika fani ya Sanaa. Mafunzo hayo yamewezesha Watoto kukuza vipaji, kujengeka kimaadili na kuimarisha weledi wa utamaduni. Aidha, Mafunzo ya Sanaa na Ujasiriamali yametolewa kwa wasanii 100 katika Wilaya

ya Tabora Mjini ambayo yamewawezesha kuanzisha miradi mbalimbali ya kisanaa itakayowasaidia kujiufigiri na kuinua kipato chao.

- 45. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarishe ushirikiano na wadau wa Sanaa, BASATA limeendesha midahalo 30 ya Jukwaa la Sanaa kwa wasanii, waandishi wa habari na wadau wa sanaa wapatao 3,000. Kutokana na midahalo hiyo, Wasanii wameweza kupata ujuzi wa kufanya kazi zao za kisanii na kupata fursa za kuboresha sanaa zao. Aidha, Waandishi wa Habari wamepata fursa ya kupata habari za sanaa kutoka kwa wahusika. Pia, Baraza limeendelea kufanya usajili wa wadau wa sanaa na wasanii wapatao 348 wanaojishughulisha na kazi za sanaa katika Mikoa ya Dar es Salaam (236), Arusha (46), Mwanza (11), Morogoro (12) na Mbeya (43).
- 46. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuwa na utaratibu mzuri wa upatikanaji wa takwimu za kazi za sanaa, BASATA imekamilisha mfumo wa kanzi data na imeendelea na zoezi la uingizaji wa taarifa za kumbi zilizosajiliwa katika mfumo huu.

- 47. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha fani ya sanaa, BASATA ilitoa elimu ya urasimishaji wa muziki kwa wasanii na wadau wa Sanaa 927 ambapo wasanii 427 ni kuitia programu ya Jukwaa la Sanaa na wasanii 500 katika Semina ya ‘Siku ya Msanii’.
- 48. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2014/2015 Bodi ya Filamu ilishiriki kikamilifu katika urasimishaji wa Tasnia ya Filamu, ambapo hadi kufikia Aprili, 2015 jumla ya stempu 22,990 zilitolewa. Kati ya hizo 18,420 zilitolewa kwa kazi za filamu ilihali 4,570 zilitolewa kwa kazi za muziki. Urasimishaji huo, umewezesha kupata takwimu za Tasnia ya Filamu na kubaini kazi halisi zinazoingizwa sokoni.
- 49. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi ya Filamu ilikagua jumla ya filamu 654 na kuziwekea madaraja. Kati ya hizo, filamu 593 zilikuwa za ndani ya nchi na filamu 61 zilitoka nje ya nchi. Sambamba na ukaguzi wa filamu, Bodi imeendelea kuitia na kuitisha jumla ya miswada 110 kwa waombaji wa ndani na nje ya nchi.

- 50. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi ya Filamu kwa kushirikiana na wataalam wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam kupitia Idara ya Sanaa na Sanaa za Maonesho imeanza kufanya utafiti wa kubaini soko la filamu nchini ili kuboresha kazi za sanaa ziweze kuingia katika soko la ushindani la ndani na nje ya nchi.
- 51. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) iliendesha Mafunzo ya Stashahada kwa wanafunzi 238 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 255. Aidha, TaSUBa iliendelea kukamilisha mitaala ya Shahada ya Kwanza ya Sanaa za Maonesho na Sanaa za Ufundu na kuipeleka Mamlaka za juu kwa hatua za maamuzi.
- 52. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutangaza maendeleo ya taaluma ya Sanaa, Taasisi iliendesha Tamasha la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania la 33 ambalo lilifanyika mwezi Septemba, 2014. Jumla ya vikundi 47 vya Sanaa za Maonesho na vikundi 16 vya Sanaa za Ufundu vilishiriki kwenye tamasha hilo.

## SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

- 53.** *Mheshimiwa Spika*, michezo ni moja ya vichocheo muhimu katika kuimarisha umoja, mshikamano na maendeleo ya taifa kwa jumla. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, utekelezaji wa shughuli za michezo umeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ushiriki mdogo wa jamii katika michezo, uchache wa miundombinu kulingana na mahitaji halisi na upungufu wa wataalam wa michezo.
- 54.** *Mheshimiwa Spika*, katika jitihada za kukabiliana na changamoto zilizopo, mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Mafunzo hayo yalitolewa katika fani za Stashahada ya Elimu kwa Michezo, Stashahada ya Utawala na Uongozi na Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji wa Michezo. Aidha, mafunzo ya kutumia “Kadi za Michezo” yalitolewa kwa walimu wa Shule za Msingi, kupitia Vituo vya Michezo vya Arusha na Songea. Vilevile, mafunzo ya kuwawezesha washiriki kuboresha na kuimarisha uendeshaji wa michezo shulenii na mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA yalitolewa

katika vituo hivyo.

- 55. *Mheshimiwa Spika*,** katika jitihada za kuimarisha afya kwa wanamichezo, Wizara imeendelea kutoa huduma ya Tiba na Kinga kwa wanamichezo 373 wakiwemo wanafunzi chipukizi 200, wachezaji 52 viongozi, mashabiki na watumishi 121. Katika kudhibiti matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu katika michezo wachezaji 10 walichukuliwa vipimo na ikathibitishwa kwamba hawakutumia madawa hayo. Aidha, Watanzania saba walishiriki kwenye mafunzo ya kudhibiti matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu katika michezo yaliyofanyika Nairobi, Kenya.
- 56. *Mheshimiwa Spika*,** katika michezo ya kimataifa Wizara imeratibu ushiriki wa Tanzania katika Michezo ya Jumuiya ya Madola iliyofanyika mwezi Julai na Agosti 2014 huko Glasgow, Scotland.
- 57. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kusajili vyama vyta michezo ambapo vyama 13, vilabu vyta michezo 239 na vituo vyta michezo vitano vimesajiliwa. Usajili huo umeviwezesha vyama na vituo kufanya kazi zao kwa kuzingatia utawala wa sheria

na kujenga demokrasia miongoni mwa wanamichezo na jamii kwa ujumla.

- 58. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha miundombinu ya michezo nchini, Wizara imeendelea kukamilisha kazi za ukarabati wa Uwanja wa Uhuru. Aidha, katika kuboresha mazingira ya watumishi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Wizara imefanya ukarabati mkubwa wa nyumba nne (4) za watumishi wa Chuo hicho ili kutoa makazi bora na maendeleo ya taaluma kwa ujumla.
- 59. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza la Michezo la Taifa limeendelea kuimarisha ushiriki wa wananchi katika michezo kwa kufundisha walimu wapatao 200 kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa kupitia Mpango wa Michezo Jumuishi kwa Jamii. Mpango huu unalenga kupata walimu wa kufundisha michezo katika jamii na kusisimua maendeleo ya michezo miongoni mwa wananchi.

**60. *Mheshimiwa Spika*,** Baraza pia limeratibu na kuwezesha shughuli mbalimbali za utawala bora katika michezo ikiwemo kuratibu na kusimamia mafunzo kwa mashirikisho saba ya michezo kuhusu mapambano dhidi ya rushwa michezoni. Aidha, Baraza liliratibu na kusimamia chaguzi kwa Vyama/ mashirikisho matano ya michezo nchini yaliyokuwa yamefikia muda wa kufanya uchaguzi.

**61. *Mheshimiwa Spika*,** Baraza liliendesha mikutano ya wadau kuwaelimisha kuhusu kutumia mifumo rasmi ya michezo katika kutekeleza programu zao za Maendeleo ya Michezo. Mifumo hiyo ilipatikana baada ya kuunganisha programu mbalimbali za mafunzo ya Vyama vya Michezo vya Taifa.

## **UTAWALA NA MENEJIMENTI YA RASILIMALI WATU**

**62. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuwawezesha watumishi kuongeza tija sehemu za kazi, katika kipindi cha mwaka 2014/2015 Wizara imewajengea uwezo watumishi 17 kwa kuwapeleka katika mafunzo mbalimbali ya muda mrefu. Aidha, Watumishi 150

walihudhuria mafunzo ya muda mfupi kuhusu elimu ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa sehemu ya kazi.

- 63. *Mheshimiwa Spika*,** kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma toleo la mwaka 1999 na 2008 pamoja na taarifa za Upimaji Kazi wa Wazi (OPRAS), Wizara imeendelea kusimamia stahili na haki za Watumishi kwa kuwapandisha vyeo Watumishi 23 wenye sifa zinazostahili.
- 64. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendeleza juhudzi za kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa watumishi na kuwahamasisha kujitokeza kupima afya zao. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa msaada wa chakula na lishe kwa Watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI ambao wamejitokeza.

#### **D. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

##### **SEKTA YA HABARI.**

- 65. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuisemea Serikali katika masuala muhimu yanayohitaji ufanuzi na kuratibu Vitengo vya Mawasiliano Serikalini;
- (ii) Kukusanya, kuandika na kusambaza habari mbalimbali za matukio ya Serikali kwa wananchi kupitia vyombo vya Habari;
- (iii) Kupiga picha za matukio mbalimbali ya Serikali, kuzisambaza katika vyombo vya habari na kuzihifadhi katika makavazi ya Idara;
- (iv) Kusajili magazeti na machapisho na kuwapatia vitambulisho waandishi wa habari wanaostahili na
- (v) Kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Habari kwa Umma.

**66. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2015/2016 TBC imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kurusha matangazo ya vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (ii) Kuandaa vipindi vya kuelimisha jamii kuhusu Katiba Inayopendekezwa na Uchaguzi Mkuu;
- (iii) Kurusha matangazo ya matokeo ya chaguzi mbalimbali na sherehe za kuwaapisha Viongozi;
- (iv) Kuandaa vipindi vya kuelimisha umma

- kuhusu matukio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na
- (v) Kulipia huduma ya kukodi “satellite” kwa ajili ya kurushia matangazo ya televisheni na redio.

**67. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuendelea na mchakato wa mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji;
- (ii) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa mradi wa kuendeleza kiwanja kilichopo kitalu na. 27, Central Business Park Dodoma unaofanyika kwa ubia kati ya TSN na TCRA;
- (iii) Kuboresha maktaba ya Kampuni;
- (iv) Kufanya mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi ili kuongeza tija kwa Kampuni;
- (v) Kuboresha maudhui ya Magazeti ya Serikali na
- (vi) Kutoa machapisho maalumu kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu Katiba Inayopendekezwa na Uchaguzi Mkuu.

**68. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara kupitia Kamati ya Maudhui ya Utangazaji imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kufuatilia kwa karibu maudhui ya vituo vyote vya utangazaji vikiwemo vile vya mikoani na vijiji ili kuhakikisha matangazo yanayorushwa yanazingatia Sera, Sheria, Kanuni na masharti ya leseni za utangazaji na
- (ii) Kuendelea kuvifatilia vituo hivi ili kuhakikisha vinaajiri watendaji wenyewe weledi katika masuala ya utangazaji na wanakuwa na mikataba ya ajira.

## **SEKTA YA MAENDELEO YA VIJANA**

**69. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya Vituo vya vijana (Ilonga, Sasanda na Marangu);
- (ii) Kuwajengea uwezo vijana kupitia vikundi vyao kwa kuendelea kuwapatia mikopo na mafunzo mbalimbali;
- (iii) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru nchini na
- (iv) Kuendelea na uratibu wa uanzishwaji wa Baraza la Vijana Tanzania.

## **SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI**

**70.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara kupitia sekta hii itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kukuza na kuendeleza matumizi sanifu na fasaha ya lugha ya Kiswahili;
- (ii) Kuandaa na kuendesha Mkutano Mkuu wa Sekta ya Utamaduni kwa kushirikiana na wadau;
- (iii) Kufanya utafiti wa mila na desturi katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma;
- (iv) Kusimamia utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na
- (v) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Jumba la Utamaduni Bagamoyo.

**71.** *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuandaa vipindi 52 vya lugha ya Taifa kupitia redio ya TBC<sub>Taifa</sub>, vipidi 52 vya Kumepambazuka kupitia Radio One na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili kupitia televisheni ya TBC<sub>1</sub>;
- (ii) Kufanya tafsiri kwa asasi za serikali, mashirika ya umma na ya binafsi pamoja na watu binafsi;

- (iii) Kufanya ukarabati mkubwa wa jengo moja la ofisi na
- (iv) Kuandaa kanuni za kiutumishi za Baraza.

**72. *Mheshimiwa Spika*,** Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuendelea na usajili wa wasanii na wadau wanaojishughulisha na shughuli za sanaa;
- (ii) Kuendesha mafunzo ya ngoma za asili kwa watoto 80 na walimu 20 wa shule za msingi katika Wilaya ya Masasi Mkoani Mtwara;
- (iii) Kuboresha Tovuti ya BASATA [www.basata.go.tz](http://www.basata.go.tz) na kuiunganisha na mitandao ya kijamii na
- (iv) Kutoa elimu na kuwajengea uwezo viongozi wa vikundi 50, vyama 30 na mashirikisho manne ya sanaa.

**73. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2015/2016, TaSUBa inakusudia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa washiriki 310 na mafunzo ya muda mfupi

- kwa wasanii 150 walio kazini;
- (ii) Kuendesha mafunzo ya cheti cha NTA-4 katika fani ya uzalishaji na usanifu wa muziki kwa washiriki 15;
  - (iii) Kufuatilia upatikanaji wa ithibati na usajili kutoka NACTE kwa ajili ya kuanza kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza ya Sanaa za Maonesho na Ufundı;
  - (iv) Kuendeleza programu za kubadilishana uzoefu kati ya TaSUBa na Chuo Kikuu cha Stavanger, Shule ya Utamaduni nchini Norway na Shule ya Sanaa ya mji wa Utercht nchini Uhlanzi na
  - (v) Kuendesha Tamasha la 34 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania.

**74. *Mheshimiwa Spika*,** Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2015/16 Bodi ya Filamu imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo :-

- (i) Kupitia miswada 165 ya kutengeneza Filamu na kutoa vibali;
- (ii) Kukagua na kuwekea madaraja filamu 600 na kuzitolea vibali pamoja na kuendesha operesheni dhidi ya filamu zitakazoingia sokoni bila kufuata taratibu;
- (iii) Kutoa mafunzo ya kujenga uelewa kwa

- Sekretarieti za Bodi za Mikoa na Wilaya katika kanda nne za Tanzania bara;
- (iv) Kuendelea kuboresha urasimishaji wa Tasnia ya Filamu na
  - (v) Kuandaa na kuendesha vipindi 25 vya elimu kuhusu masuala ya filamu.

## **SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO**

**75. *Mheshimishwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuratibu ushiriki wa timu za Taifa katika Michezo ya Afrika itakayofanyika Brazaville, Kongo mwezi Septemba 2015;
- (ii) Kuendesha mafunzo ya utalaamu wa Michezo;
- (iii) Kutoa huduma ya Kinga na Tiba kwa Wanamichezo na wadau wa michezo;
- (iv) Kusajili Vyama na Vilabu vya Michezo na
- (v) Kuendeleza miundombinu ya Michezo nchini.

**76. *Mheshimiwa spika*,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2015/2016, Baraza la Michezo la Taifa limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuendesha mafunzo ya utawala Bora na mapambano dhidi ya Rushwa Michezoni;
- (ii) Kuratibu na kusimamia chaguzi za Vyama sita vya Michezo vilivypanga kufanya uchaguzi;
- (iii) Kuratibu Mkutano Mkuu wa Kamati za Michezo za Mikoa yote Tanzania Bara na
- (iv) Kuendelea kuhamasisha wananchi wote kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo.

## **UTAWALA NA MENEJIMENTI YA RASILIMALI WATU**

**77. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuendelea kuhamasisha Watumishi kukubali kupimwa VVU/UKIMWI kwa hiari ili kutambua hali zao na kuendelea kutoa msaada wa chakula na lishe kwa Watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI ambao wamejitokeza;
- (ii) Kuendelea kuimarisha Utawala bora kwa kushirikisha Watumishi sehemu za kazi kwa kuendesha vikao mbalimbali vya kiutawala na Baraza la Wafanyakazi;

- (iii) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa katika mpango wa mafunzo na
- (iv) Kuhakikisha Watumishi wote wenye sifa na wanaostahili wanapandishwa vyeo kwa kuzingatia miundo ya kada zao, Sera ya Menejimenti katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na 2008 na taarifa ya Utendaji Kazi wa Wazi (OPRAS).

## E: HITIMISHO

**78. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili Sekta hizo ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Hii ni pamoja na kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kutoa habari, kulinda mila na desturi, kudumisha amani na mshikamano katika jamii. Wizara itaendelea kukabiliana na changamoto zilizoainishwa katika hotuba hii, ili zipatiwe ufumbuzi na hatimaye fursa zinazopatikana katika Sekta za Wizara ziweze kutumika ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi. Napenda kuwahakikishia

wananchi ya kwamba Wizara ina nia thabiti ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo hatua kwa hatua kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi.

## SHUKRANI

- 79. *Mheshimiwa Spika*,** kwa niaba ya Serikali na kwa niaba yangu binafsi naomba kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 katika kutimiza malengo yetu. Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yamepatikana kutokana na ushirikiano uliopo mionganini mwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara.
- 80. *Mheshimiwa Spika*,** shukrani zangu za pekee ziende kwa **Mhe. Alhaji Juma Suleiman Nkamia** (Mb.), Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; **Bibi Sihaba Nkinga**, Katibu Mkuu na **Prof. Elisante Ole Gabriel**, Naibu Katibu Mkuu. Ninawashukuru kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kikamilifu tangu nilipoteuliwa na Mhe. Rais kuiongoza Wizara hii. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wakurugenzi

Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Watendaji Wakuu wa Asasi, Wataalamu na Watumishi wote wa Wizara kwa juhudi wanazofanya kuhakikisha kuwa Taifa letu linahabarishwa vizuri, lina vijana wenye uwezo na malezi bora, linathamini utamaduni wake na linakuwa mahiri katika michezo ifikapo mwaka 2025.

- 81. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kuzishukuru Bodi na Asasi za Wizara kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Shukrani za kipekee ziende kwa wenyeviti na wajumbe wa Bodi za Asasi hizo kwa kuweza kuzisimamia, kuziongoza na kuzishauri kikamilifu kwa niaba ya Serikali. Wenyeviti hao ni pamoja na: **Prof. Mwajabu Possi** – TBC; **Prof. Moses Warioba** – TSN; **Prof. Penina Mlama** – BASATA; **Prof. Martha Qorro** – BAKITA; **Bw. Ghonche Materegho** – TaSUBa na **Bw. Sylvester Sengerema** – Bodi ya Filamu. Wengine ni **Bw. Dionis Malinzi** – BMT na **Bw. Christopher Gachuma** – Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Bodi na Asasi hizo zimeisaidia Serikali kuendelea kuwatumikia wananchi wake kwa uadilifu na weledi mkubwa.

**82. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao wameshirikiana nasi wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Wizara. Siyo rahisi kuwataja wote lakini nitaje wachache ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Japan, Norway, Iran, Ethiopia, New Zealand, Turkey, Korea ya Kusini, Marekani, Ujeruman, India na Sri-lanka. Vilevile tumeshirikiana na Mashirika ya Kimataifa ambayo ni pamoja na: UNESCO, UNICEF, UNFPA, UNDP, UNV, ILO, JICA, KOICA, CYP, ESAMI, RALEIGH INTERNATIONAL, VSO, AMREF, IYF, BRAC, BRITISH COUNCIL, Restless Development, Balton Tanzania Limited na Kampuni ya Ak'Omungoma. Aidha, yapo makampuni ya ndani ambayo yanajumuisha TBL, Serengeti Breweries, Coca Cola, Vodacom, Airtel, Zantel, Tigo, TTCL, Azam na tsn. Vilevile zipo Asasi za kifedha za NMB Bank, CRDB Bank, Exim Bank, Standard Charter Bank na Mifuko ya hifadhi ya jamii ya NSSF, PSPF na PPF.

**83. Mheshimiwa Spika**, navishukuru Vyombo vya Habari nchini kwa kazi nzuri ya kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha umma. Ni matumaini yangu kwamba

Vyombo hivi vitatumika kikamilifu katika kuhabarisha na kuwaelimisha wananchi juu ya matukio makubwa ya kitaifa yaliyo mbele yetu ya uchaguzi mkuu pamoja na Katiba Inayopendekezwa. Aidha, ninamshukuru Mchapaji wa Kitabu hiki ambaye ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati. Vilevile navishukuru vituo vya televisheni na redio ambavyo vinarusha hotuba hii hewani moja kwa moja.

## **MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

### **Mapato**

**84. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imepanga kukusanya shilingi **1,330,008,000** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Mchanganuo wa makusanyo kifungu kwa kifungu kwa mwaka 2014/2015 na Makadirio kwa mwaka 2015/2016 upo katika **Kiambatisho Na. I.**

### **Matumizi ya Kawaida**

**85. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imetengewa shilingi **24,413,548,000** kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha:-

- (i) Mishahara ya Wizara shilingi  
**4,034,340,000**
- (ii) Mishahara ya Asasi shilingi  
**12,883,139,000**
- (iii) Matumizi Mengineyo ya Wizara shilingi  
**4,456,069,000**
- (iv) Matumizi Mengineyo ya Asasi shilingi  
**3,040,000,000**

Mchanganuo wa makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Asasi upo katika **Kiambatisho Na. II.** Matumizi ya Kawaida kwa Wizara peke yake rejea **Kiambatisho Na. III** na kwa Asasi rejea **Kiambatisho Na. IV.**

### **Miradi ya Maendeleo**

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imetengewa jumla ya shilingi **5,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo kamili upo katika **Kiambatisho Na. V.**

## **MAOMBIYAFEDHAKWAAJILYAKUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2015/2016.**

- 87. Mheshimiwa Spika**, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2015/2016, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi **29,413,548,000** ambapo kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi **24,413,548,000** na Fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi **5,000,000,000**. Mchanganuo wa fedha hizi upo katika viambatisho vilivyotajwa hapo awali ambavyo ni sehemu ya Hotuba hii.
- 88. Mheshimiwa Spika**, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz) na [www.tanzaniangovernment.blogspot.com](http://www.tanzaniangovernment.blogspot.com).
- 89. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

## F. VIAMBATISHO

*Kiambatisho Na. I*

### MAKUSANYO YA MAPATO MWAKA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MWAKA 2015/2016 (Sh)

#### **Idara ya Utawala na Rasilimali Watu**

Na	Code ya Mapato	Maelezo	Makisio ya Mapato 2014/2015	Makusanyo Julai hadi Aprili, 2015	Makadirio ya 2015/2016
1	2	3	4	5	6
1.	140283	Mauzo ya Zabuni	1,000	-	1,000
2.	140368	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	1,000	-	1,000
3.	140370	Marejesho ya fedha za Umma	1,000	-	1,000
<b>JUMLA NDOGO</b>			<b>3,000</b>	<b>-</b>	<b>3,000</b>

#### **Idara ya Utamaduni**

1.	140312	Ukaguzi wa filamu	50,000,000	88,062,126	65,000,000
2.	140370	Marejesho ya fedha za Umma	-	-	-
3.	140368	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	-	-	-

4.	140386	Vibali vya kutengeneza filamu	400,000,000	326,365,542	450,000,000
<b>JUMLA NDOGO</b>			<b>450,000,000</b>	<b>414,427,668</b>	<b>515,000,000</b>

**Idara ya Michezo**

1.	140259	Mapato ya viwanja vya Michezo (Uhuru na Taifa)	560,000,000	343,261,368	640,000,000
2.	140315	Ada za Mafunzo	35,000,000	-	40,000,000
3.	140370	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	1,000	-	1,000
4	140370	Marejesho ya fedha za Umma	1,000	-	1,000
<b>JUMLA NDOGO</b>			<b>595,002,000</b>	<b>343,261,368</b>	<b>680,002,000</b>

**Idara ya Habari**

1.	140202	Machapisho ya picha, mabango na majarida	35,000,000	4,645,000	50,000,000
2.	140264	Usajili wa magazeti	25,000,000	15,530,400	30,000,000
3.	140265	Ada ya kuijunga		-	
4.	140265	Ukumbi wa mikutano	24,000,000	12,840,000	30,000,000
5.	140310	Ada ya mwaka ya Magazeti	1,000	-	1,000
6.	140368	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	1,000	-	1,000

7.	140370	Marejesho ya fedha za Umma	1,000	-	1,000
8.	140387	Vitambulisho vya Waandishi wa Habari	20,000,000	20,911,680	25,000,000
<b>JUMLA NDOGO</b>			<b>104,003,000</b>	<b>53,927,080</b>	<b>135,003,000</b>
<b>JUMLA KUU</b>			<b>1,149,008,000</b>	<b>811,616,116</b>	<b>1,330,008,000</b>

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo – Kitengo cha Fedha na Uhasibu

**Kiambatisho**

**Na. II**

**MUHTASARI WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA 2015/2016  
WIZARA NA ASASI**

IDARA/KITENGO	MAKISIO 2015/2016		
	MISHAHARA (PE)	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA (3+4)
(1)	(2)	(3)	(4)
1001-UTAWALA NA RASILIMALI WATU	1,193,587,000	1,960,442,000	3,154,029,000
1002 – FEDHA NA UHASIBU	240,705,000	47,440,000	288,145,000
1003 – SERA NA MIPANGO	226,536,000	157,260,000	383,796,000
1004-MAWASILIANO SERIKALINI	47,245,000	28,106,000	75,351,000
1005- UNUNUZI NA UGAVI	149,404,000	67,150,000	216,554,000
1006- UKAGUZI WA NDANI	87,221,000	50,978,000	138,199,000
1007- TEHAMA	64,729,000	102,921,000	167,650,000

1008 - SHERIA	28,488,000	22,102,000	50,590,000
6001 – MAENDELEO YA UTAMADUNI	4,217,774,000	749,202,000	4,966,976,000
6002 – MAENDELEO YA VIJANA	415,171,000	647,095,000	1,062,266,000
6004 – MAENDELEO YA MICHEZO	1,371,334,000	2,322,466,000	3,693,800,000
7003 – HABARI	8,875,285,000	1,340,907,000	10,216,192,000
<b>JUMLA KUU</b>	<b>16,917,479,000</b>	<b>7,496,069,000</b>	<b>24,413,548,000</b>

**Chanzo:** Wizara ya Fedha – Machi, 2015

## MUHTASARI WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA 2015/2016 – WIZARA

IDARA/KITENGO	MAKISIO 2015/2016		
	MISHAHARA (PE)	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA (2+3)
(1)	(2)	(3)	(4)
1001-UTAWALA NA RASILIMALI WATU	1,193,587,000	1,960,442,000	3,154,029,000
1002 – FEDHA NA UHASIBU	240,705,000	47,440,000	288,145,000
1003 – SERA NA MIPANGO	226,536,000	157,260,000	383,796,000
1004-MAWASILIANO SERIKALINI	47,245,000	28,106,000	75,351,000
1005-UNUNUZI NA UGAVI	149,404,000	67,150,000	216,554,000
1006-UKAGUZI WA NDANI	87,221,000	50,978,000	138,199,000
1007- TEHAMA	64,729,000	102,921,000	167,650,000
1008 - SHERIA	28,488,000	22,102,000	50,590,000
6001 -UTAMADUNI	425,273,000	289,202,000	714,476,000
6002 - VIJANA	415,171,000	647,095,000	1,062,266,000

6004 – MICHEZO	581,917,000	742,466,000	1,324,383,000
7003 – HABARI	574,064,000	340,907,000	914,971,000
<b>JUMLA</b>	<b>4,034,340,000</b>	<b>4,456,069,000</b>	<b>8,490,409,000</b>

**Chanzo:** Wizara ya Fedha – Machi, 2015

## MUHTASARI BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA 2015/2016 – ASASI

TAASISI/MASHIRIKA	MAKISIO YA 2015/2016		
	MISHAHARA (PE)	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA (2+3)
(1)	(2)	(3)	(4)
6001-280514 BODI YA FILAMU.	-	190,000,000	190,000,000
6001- 280515 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)	1,210,733,000	90,000,000	1,300,733,000
6001-280516 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)	771,137,000	90,000,000	861,137,000
280328 – TaSUBa	1,810,631,000	90,000,000	1,900,631,000
6004 – 280518 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)	789,417,000	90,000,000	879,417,000

6004 – 280518 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (MAKOCHEA)	-	1,230,000,000	1,230,000,000
6004 – 270380 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO-MALYA	-	220,000,000	220,000,000
6004 – 270839 KITUO CHA MICHEZO – ARUSHA	-	20,000,000	20,000,000
6004 – 270840 KITUO CHA MICHEZO- SONGEA	-	20,000,000	20,000,000
7003 – 280577 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)	8,301,221,000	1,000,000,000	9,301,221,000
<b>JUMLA</b>	<b>12,883,139,000</b>	<b>3,040,000,000</b>	<b>15,923,139,000</b>

**Chanzo:** Wizara ya Fedha – Machi, 2015

## BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO 2015/2016

MRADI	MAKADIRIO YA 2015/2016		
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	JUMLA
<b>6001 – IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI</b>			
6246-Ujenzi wa Ofisi Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)	500,000,000	-	500,000,000
6293-Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika	250,000,000	-	250,000,000
6355-Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonyesho ya Sanaa (BASATA)	1,000,000,000	-	1,000,000,000
<b>Jumla</b>	<b>1,750,000,000</b>	-	<b>1,750,000,000</b>
<b>6002 – IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA</b>			
4945- Mfuko wa Maendeleo wa Vijana	1,500,000,000	-	1,500,000,000
6380- Ukarabati wa Vituo vya Vijana	200,000,000	-	200,000,000
<b>Jumla</b>	<b>1,700,000,000</b>	-	<b>1,700,000,000</b>
<b>6004 – IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO</b>			
6385-Ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya	250,000,000	-	250,000,000

6523-Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo	250,000,000	-	250,000,000
<b>Jumla</b>	<b>500,000,000</b>	-	<b>500,000,000</b>
<b>7003 – IDARA YA HABARI</b>			
4279 - Upanuzi na Usikivu wa TBC	1,000,000,000	-	1,000,000,000
6567 - Habari kwa Umma	50,000,000		50,000,000
Jumla	1,050,000,000	-	1,050,000,000
<b>JUMLA KUU</b>	<b>5,000,000,000</b>	-	<b>5,000,000,000</b>

**Chanzo:** Wizara ya Fedha – Machi, 2015